



MGAO WA HAKI KWA WANAWAKE: KUFANIKISHA FIDIA NA MAKAZI MAPYA KWA USAWA ZAIDI NCHINI TANZANIA NA MSUMBIJI

CELINE SALCEDO-LA VIÑA NA LAURA NOTESS

MUHTASARI MKUU

Mambo Muhimu

- Wanawake wanakumbwa na athari mbaya za uwekeza-aji mkubwa wa ardhi (katika kilimo biashara, utumizi wa rasilimali, ukataji miti) katika maeneo ya Kusini mwa ulimwengu.
- Ukosefu wa haki rasmi za kisheria na cheo chao cha chini katika kaya na jamii kunapelekea wanawake kutengwa katika michakato ya kufanya maamuzi na kuwapuuza katika kutoa fidia na mipango ya kupanga na kutekeleza uhamisho kwenye makazi mapya.
- Nchi mbili zinazokuza uwekezaji wa biashara ya ardhi, Tanzania na Msumbiji, sheria zinahitaji mashauriano kufanya na jamii na jamii zinazoathirika kulipwa fidia, lakini zinakosa kuangazia wasiwasi na mitazamo ya wanawake vya kutosha. Mapengo katika sheria yanajumuisha kukosa kuzingatia mahitaji ya ardhi na shughuli za ukulima za wanawake na hitaji yao ya kuweza kutumia rasilimali za jamii (kama vile maji, kuni, na mimea ya mweituni) na miundombinu ya jamii ili kusaidia kujenga upya riziki zao.
- Wanawake hawawakilishwi vya kutosha katika mashirika yanayofanya maamuzi, nazo sheria zinakosa mbinu za kuhakikisha ushiriki muhimu katika mashauriano na jamii na michakato ya kupata vibali.
- Mabadiliko ya udhibiti—ikiwemo mabadiliko ya ustahiki wa kufidiwa na mbinu za malipo, fungu la jinsia katika mashirika yanayofanya maamuzi, michakato ya kushiriki zaidi na mifumo ya migogoro, kuhamasisha jamii zaidi, na kufahamisha mamlaka za serikali na

wawekezaji kuhusu jinsia—yanaweza kufanya michakato ya fidia na makazi mapya kuwa ya usawa zaidi kwa wanawake.

Usuli

Tafiti zinaonyesha kwamba wanawake wana-kumbwa na athari mbaya za biashara ya ardhi katika maeneo ya Kusini mwa ulimwengu. Uwekezaji katika kilimo biashara, uchimbaji madini, na ukataji miti umepelekea jamii kupoteza ardhi na kuhamishwa, kupoteza riziki, na kupoteza rasilimali za jamii—na athari zake ni mbaya zaidi kwa wanawake ikilinganishwa na wanaume. Haki duni, viwango vikubwa vya kutojua kusoma/kuandika, na cheo chao cha chini katika jamii kunapelekea mara nyingi wanawake kutengwa katika kufanya maamuzi, kutoa fidia, na mipango ya kupanga na kutekeleza uhamisho kwenye makazi mapya. Kwa ujumla wanawake hawapokei fidia, na wanapoteza rasilimali (maji, kuni, mimea na matunda ya mweituni) ambazo wanahitaji kutumia katika kaya na ili kupata riziki ya ziada. Wanapohamishwa na kupata makazi mapya katika maeneo mapya, wanaachwa na mbinu chache za kujenga upya mifumo yao ya uzalishaji na mitandao ya kijamii.

Rasimu hii inachunguza jinsi mapengo katika sheria zinazosimamia fidia ya ardhi na makazi mapya nchini Tanzania na Msumbiji yanavyopelekea wanawake kutengwa. Inaendeleza rasimu ya hapo awali ya Taasisi ya Rasilimali Ulimwenguni (World Resources Institute, WRI), “Kuhakikisha Sauti za Wanawake Zinasikika katika Kufanya Maamuzi ya

Jamii kuhusu Uwekezaji katika Ardhi,” ambayo inachunguza mbinu za udhibiti zinazosimamia michakato ya ununujaji ardhi na inatambua njia za kuimarisha ushiriki wa wanawake katika kufanya maamuzi husika. Rasimu hii inachanganua upungufu katika kanuni zinazosimamia michakato tofauti ya fidia ya ardhi na uhamisho kwenye makazi mapya. Sawia na rasimu ya hapo awali, rasimu hii ina msingi kwenye mradi wa pamoja wa WRI, Mpango wa Kutengeneza Mitandao ya Jinsia nchini Tanzania (TGNP), Chama cha Mawakili Wanawake nchini Tanzania (TAWLA), na Centro Terra Viva (CTV) (nchini Msumbiji). WRI ilifanya uchanganuzi wa kisheria na mapitia ya fasihi, na kupata michango kutoka kwa washirika nchini; washirika hawa walifanya utafiti nyanjani, ambapo WRI ilishiriki katika baadhi ya utafiti huo. Mradi huu pia ulijumuisha shughuli za kufikia jamii zilizofanyiwa utafiti na pamoja na mashirika husika ya kitaifa na ya serikali ya kitaifa. Lengo la mradi huu ni kuwezesha wanawake kutambuliwa kama wadau katika utawala wa ardhi ya jamii na kuunda nafasi za wao kuhusishwa katika michakato ya kufanya maamuzi.

Sheria kuhusu Fidia na Makazi Mapya

Nchi za Tanzania na Msumbiji ni miongoni mwa nchi zinazolengwa zaidi katika ununuzi wa ardhi ya biashara katika maeneo ya kusini mwa Ulimwengu. Serikali katika nchi hizi mbili zinahamamisha wawekezaji, kwa misingi ya biashara ya rasilimali na kilimo. Ardhi nyingi inayokusudiwa au kutengewa wawekezaji inatambulika kisheria kuwa inamilikiwa au ni makazi ya jamii za kidehuri, na hupelekea uhamisho na migogoro kati ya jamii na wawekezaji.

Sheria za nchi hizi mbili zinahitaji fidia kulipwa wakati ardhi ya jamii inaponunuliwa. Kanuni zinazotekeleza sheria za ardhi nchini Tanzania, hususa Kanuni za Ardhi ya Kijiji za 2001, zinabainisha mahitaji na taratibu za fidia. Fidia inalipwa kwa ajili ya ardhi na maendeleo kwenye ardhi hiyo, kama vile nyumba, miti, na mazao yaliyo shambani, kulingana na mbinu zilizobainishwa za kuweka thamani. Marupurupu fulani—usumbufu, usafirishaji, malazi, na kupoteza faidi—pia huenda yakalipwa. Fidia inaweza kuwa kwa pesa taslimu; ardhi mbadala; vitu sawia (miche, nafaka, n.k.); au mchangan-yiko wa mbinu kadhaa. Hata hivyo, isipokuwa chini ya Sheria ya Uchimbaji Madini na katika miradi inayofad-

hiliwa na benki za maendeleo, utoaji ardhi mbadala ni kwa hiari, lakini si lazima. Baraza za kijiji (shirika linalosimamia kijiji) ni lazima liandikishe dai la kufiwa kwa ajili ya ardhi na rasilimali za jamii, nazo kaya zilizoathirika ni lazima ziwasilishe madai kwa ajili ya ardhi waliyo nayo. Hakuna sera, sheria wala kanuni maalum inayosimamia uhamisho kwenye makazi mapya.

Sheria za Msumbiji zinakosa miongozo tosha ya fidia. Sheria ya Ardhi ya 1997 inahitaji kwamba baada ya mwekezaji kufanya mashauriano na jamii zilizoathirika, mtawala wa wilaya atatoa maoni na kueleza kama ardhi husika ni ina watu au la na ikiwa haina watu atabainisha masharti ya “ushirikiano” yanayokubalianwa baina ya mwekezaji na jamii. Sheria haina miongozo maalum ya kubainisha masharti haya ya “ushirikiano.” Katika matukio ya ardhi kuchukuliwa na serikali, ununuzi kwa madhumuni ya rasilimali, au uhamisho kwenye makazi mapya, sheria inahitaji malipo yafanywe kwa ajili ya hasara za vipengee ambavyo vinagusika (mazao, maendeleo, n.k.) au ambavyo havigusiki (njia za usafirishaji na mawasiliano, mitandao ya kijamii, n.k.). Kwa ununuzi unaofanywa kwa ajili ya rasilimali, fidia imebainishwa katika makubaliano baina ya serikali, jamii na kampuni.

Kwa manunuzi mengine yote ya kibiashara, the Kanuni za Makazi Mapya za 2012 zinahitaji kuwepo kwa mpango kamili wa makazi mapya na mpango kamili wa hatua ya utekelezaji unaojumuisha viegezo vya fidia na bajeti. Umma kushirikiwa kwa njia ya mashauriano na kutoa maoni ni lazima. Kamati ya kiufundi inayowajumuisha wawakilishi wa serikali ya kitaifa na ya ndani na mwanachama mmoja wa “eneo husika” ina majukumu ya kusimama.

Utekelezaji Fidia na Makazi Mapya

Ukosefu wa fidia kamili, ya haki, na kwa wakati unaofaa ni lalamishi kubwa katika nchini hizi mbili. Ardhi ambayo “hautumiki” au “haina kazi” (k.m., ardhi tupu au ya malisho) mara nyingi haifidiwi, na maendeleo kama vile mazao yanakadiriwa thamani ya chini sana. Fidia ya pesa kwa kawaida inacheleweshwa na haitoshi kununua ardhi mbadala ya ukubwa sawia au yenye kiwango sawia cha uzalishaji nayo fidia isiyo ya pesa haitoshi kukidhi mahitaji ya kaya. Mara nyingi jamii

zinahitajika kuondoka kwenye ardhi kabla ya kupokea fidia kamili na kabla ya eneo wanakohamia kuwa tayari kwa makazi. Mashamba mbadala mara nyingi huwa yana rutuba ya chini, ni madogo, na yako katika maeneo yaliyo mbali sana na jamii. Manufaa yanayodhaniwa kutoka na mradi, kama vile uajiri, miundombinu, na huduma ni nadra kutimizwa; yanakuwa ahadi za mdomo tu au kwa maandishi ambayo hayana wajibu wa kisheria. Miradi ya uwekezaji inawasilishwa kwa jamii kama shughuli iliyokamilika.

Mapengo ya Kijinsia

Wasiwasi za wanawake ni nadra kuzingatiwa, katika sheria au kwa matendo. Kwa ujumla wanawake hawapokei fidia, kwa sababu fidia inalipwa kwa kaya nzima na mume ndiye ana idhini ya kuwasilisha mada na kupokea malipo kama kicha cha kaya. Baadhi ya wajane Watanzania wanalalamika kwamba jamaa za waume zao marehemu wanachukua umiliki wa fidia kulingana na sheria za kiesturi. Wanawake wanapopokea fidia, wanapokea kiasi kidogo kuliko wanaume, kwa sababu wana viwanja vidogo zaidi na mazao machache zaidi na kwa sababu mazao ya chakula (wanayopania kuvuna) mara nyingi hayafidiwi kamwe.

Kupoteza uwezo wa kutumia ardhi na misitu ya jamii—ambako rasilimali kama vile maji, kuni, chakula cha mifugo, mimea na matunda ya mwituni yanapatikana—pia kunawaathiri wanawake zaidi. Wakati rasilimali hizi hazifidiwi au mbadala yake haitolewi, au wakati fidia haiwafikii wanawake, lishe ya kaya inaweza kuathirika, na kuwabidi wanawake kutumia muda na nguvu nyingi kutimiza majukumu yako ya nyumbani.

Sawia, wakati huduma za jamii na miundombinu—kama vile barabara na vituo vya afya, na vilevile mali ambayo haigusiki kama vile njia za mawasiliano—hazifidiwi au mbadala yake haitolewi katika maeneo ya makazi mapya, uwezo wa wanawake kukabiliana na hali mpya na mara nyingi hali gumu unaathirika pakubwa. Manufaa kama vile fursa za uajiri kwa kawaida zinachukuliwa na wanaume, ingawa wakati mwingine wafanyakazi wanawake wanapendelewa katika makujumu yanayohitaji ujuzi wa chini. Kwa ujumla, kulingana na mambo mengi yanayowakabili, wanawake wana machaguo machache kuliko wanaume ya kuweza kurejesha riziki au rasilimali walizopoteza.

Wanawake hawawakilishwi vya kutosha katika mashirika yanayofanya maamuzi, nazo sheria zinakosa mbinu za kuhakikisha ushiriki wao muhimu. Kutokana na hilo, wanawake wanapata ugumu wa kutekeleza haki zozote walizo nazo. Nchini Tanzania mafungu ya jinsia katika mashirika yanayosi-mamia kijiji yanatoa jukwaa la wanawake kuhusishwa katika mchakato wa ununuzi wa ardhi. Mbinu za ziada, kama vile mahitaji ya akidi na kupiga kura, zinahitajika ili kuhakikisha kwamba sauti zao zinasikika. Nchini Msumbiji, kamati ya kiufundi iliyo na majukumu msingi ya kusimamia uhamisho kwenye makazi mapya haina wajibu wa kuhakikisha wanawake wanawakilishwa, nayo wizara ya jinsia haihitajiki kutoa maoni kwenye mpango wa makazi mapya. Kanuni ziko bayana kwamba makundi ya wanaoweza kukandamizwa kama vile wajane, kaya zinazoongozwa na wanawake, wakongwe, na vijana ni lazima wasikilizwe. Lakini ushiriki wa wanawake ni lazima uwe na msingi unaozidi uwezekano wa kukandamizwa na uzingatiwe kulingana na uwepo wao na michango yao kama wadau.

Kinjisia

Ni lazima nchi ya Tanzania na Msumbiji zishughulike upungufu katika sheria ili kuhakikisha haki kwa wanawake na jamii zao. Ikiongozwa na misi-mamo muhimu ya haki za binadamu—kama vile usawa wa jinsia, mchakato kamili, ridhaa ya ufahamu ya mapema na bila malipo, na fidia—kanuni kuhusu fidia na makazi mapya zinapaswa kushughulikia masuala yafuatayo:

Fidia:

- Fidia kwa wanandoa wote wawili au kwa jamaa wote wa kaya ambao wanahusika na ardhi iliyonunuliwa na mwekezaji inapaswa iwe lazima. Mbinu za kugawa—kama vile malipo kwa majina yote mawili ya wanandoa au moja kwa moja kwa wanawake, kwa mfano kupitia huduma za fedha kwenye simu—ni lazima ziwekwe. Ardhi mbadala ni lazima iwe kwa majina ya wanandoa wote wawili.
- Malipo kwa ajili ya kupoteza uwezo wa kutumia rasilimali na mali isiyogusika ya jamii na/au mbadala yake ni lazima yafanywe kuwa ya lazima, huku kutoa mbadala ikiwa chaguo la kwanza. Miongozo ya ukadiriaji thamani ya mali ni lazima ijumuishe fidia kwa ajili ya matumizi na manufaa ambayo wanawake wanapata kutokana na rasilimali za jamii.

- Ni lazima fidia ifanywe sio tu kwa ajili ya mazao ya kibiashara (ambayo sanasana yanapandwa na wanau-me) lakini pia kwa ajili ya mazao ya chakula (ambayo sanasana yanapandwa na wanawake).
- Ni lazima ahadi za fursa za uajiri, huduma za jamii, na miundombinu iwe kwa maandishi katika hati yenye wajibu wa kisheria au vinginevyo zijumuishwe rasmi katika mpango wa fidia au makazi mapya. Ni lazima ahadi hizi zifuatwe na mipango wazi ya utekelezaji ba ratiba ya kukamilishwa kwake, na vilevile uwajibikaji kwa utekelezaji.

Uwakilishi na ushiriki wa wanawake:

- Uwakilishi wa wanawake katika mashirika na mi-chakato ya kufanya maamuzi inayohusiana na fidia na makazi mapya unaweza kufanikishwa kupitia mafun-gu ya jinsia na mahitaji ya akidi na kupiga kura katika mashirika husika yanayosimamia kijiji na mashirika ya kitaifa na enyeji, ikiwa ni pamoja na baraza la kijiji nchini Tanzania na Kamati ya Kiufundi ya Kufuatilia na Kusimamia Makazi Mapya nchini Msumbiji.
- Ushiriki munimu wa wanawake katika mashauriano yote ya jamii na majukwaa yote ya maoni ya umma unaweza kuongezewa kwa kuzingatia vizuizi vya kita-maduni, masuala ya uwezo wa kusoma/kuandika na vikwanzo vya muda na usafiri, ikiwa ni pamoja na ku-fanya mikutano ya wanawake pekee au majadiliano ya makundi na kuratibu mikutano kwenye siku ambazo ni rahisi kwa wanawake kupatikana ili kuhudhuria.
- Michango ya mashirika husika ya serikali, hususa wiz-ara inasimamia jinsia au wanawake, na vilevile jamii ya wanaharakati ni lazima ijumuishwe kupitia maobi ya maoni au ushiriki katika michakato yenyewe.
- Kampeni za hamasisho kuhusu haki na za kufaha-misha kwa jamii zinazoathirika au wenyeji ni lazima zijumuishe shughuli za kuwafikia wanawake na za kuwahamaisha wanaume.

- Mikakati ya kufuatilia na kupunguza dhuluma za kijinsia, hasa na walinzi wa makampuni, ni lazima iwe sehemu ya mipango ya makazi mapya au kutolewa katika hati tofauti kwa maadishi ya kisheria.
- Mbinu za kusuluhisha migogoro ni lazima iweze kufikika, ya haki na uwazi, mwafaka kitamaduni, na inayozingatia jinsia.

Mfumo wa kitaasisi na kiutawala wa serikali ni lazima uimarishwe kupitia shughuli za mafunzo ya jinsia na uhamasisho, mbinu za ushirikiano bora katika taasisi, na uwazi na uwajibikaji zaidi. Serikali zina jukumu muhimu katika kuunda nafasi za mabadiliko katika jamii kupitia sheria na kanuni za usawa wa jinsia ambazo zinatekelezwa katika njia zinazozingatia jinsia.

Orodha ya Mafupisho

CTV	Centro Terra Viva
DUAT	Direito de Uso e Aproveitamento da Terra
PRAI	Misimamo ya Uwekezaji Mzuri katika Kilimo na Mifumo ya Chakula
TAWLA	Chama cha Mawakili Wanawake nchini Tanzania
TGNP	Mpango wa Kutengeneza Mitandao ya Jinsia nchini Tanzania
VGGT	Miongozo ya Hiari kwa Usimamizi Mzuri wa Umiliki wa Ardhi, Maji yenye Samaki, na Misititu